

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI NA NNE



20 APRILI, 2018

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI NA NNE – TAREHE 20 APRILI, 2018

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**III. MASWALI:**

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**109. MHESHIMIWA DEOGRATIAS FRANCIS NGALAWA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Serikali iliamua pamoja na mambo mengine ya kulinusuru Shirika la Posta kuhamisha jukumu la kulipa pensheni za Wastaifu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu

la Afrika Mashariki kwenye mojawapo ya Mifuko ya Pensheni:-

Je, Serikali itakuwa tayari kuhamisha jukumu hili kwenye mojawapo ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

#### **110. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Benki ya Kilimo ipo kwa ajili ya kumuwezesha Mkulima wa Tanzania aweze kufanya uwekezaji wenyewe tija katika kilimo:-

- (a) Je, ni lini Serikali itapeleka Benki ya Kilimo katika Mkoa wa Ruvuma ili Wananchi waweze kukopeshwa;
- (b) Je, Serikali ipo tayari kupunguza riba kwa pesa anayokopeshwa Mkulima kutoka katika Benki hiyo.

#### **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

#### **111. MHESHIMIWA TWAHIR AWESU MOHAMED (MKOANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Jeshi la Polisi lina dhamana

kubwa ya kulinda usalama wa raia na mali zao na ni msimamizi mkuu katika Haki za Binadamu:-

- (a) Je, lini Jeshi hilo litafanya kazi zake kisayansi zaidi na kuondokana na kutumia nguvu zisizo za lazima wakati wa kutekeleza majukumu yake;
- (b) Je, suala la weledi kwa Watendaji wa Polisi linasimamiwa vipi ili Polisi waweze kupambana na uhalifu unaokuwa kitaalam kila siku.

#### **WIZARA YA KILIMO:**

#### **112. MHESHIMIWA KITETO ZAWADI KOSHUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Uzalishaji wa Pamba Mkoani Mwanza umepungua kutoka tani 350,000 kwa mwaka 2009 hadi tani 120,000 kwa mwaka 2016:-

Je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi ili kulifufua zao hilo.

## **WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

### **113. MHESHIMIWA QAMBALO WILLY QULWI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa ardhi yote ya Tanzania inapangwa, inapimwa na kumilikishwa kisheria kama namna mojawapo ya kuondoa migogoro hususan ya Wakulima na Wafugaji nchini.

### **114. MHESHIMIWA NJALU DAUDI SILANGA (ITILIMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Shirika la Nyumba lilianzishwa kwa ajili ya kusaidia Watumishi wa Umma pamoja na Wananchi wenyewe maisha ya chini na Mkoa wa Simiyu ni mpya ambapo tayari kuna Watumishi wengi ambaao hawana nyumba za kuishi ikiwemo Wilaya ya Itilima na Busega:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba katika Mkoa mpya wa Simiyu pamoja na Wilaya zake kwa kutumia Shirika la Nyumba.

### **WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

#### **115. MHESHIMIWA ZUBEDA HASSAN SAKURU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya muda mrefu katika kuimarisha ushiriki wenye tija kwa Tanzania katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa.

### **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

#### **116. MHESHIMIWA MARIA NDILLA KANGOYE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:- Kumekuwa na changamoto nyingi katika uvubi wa Ziwa Victoria unaosababisha malalamiko mengi kutoka kwa wadau wa uvubi:-

Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha inamaliza malalamiko hayo.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

*(Majadiliano yanaendelea)*

DODOMA  
20 APRILI, 2018

S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE



BUNGE LA TANZANIA